

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS



Ofisi ya Rais,
Ikulu,
1 Barabara ya Barack Obama,
11400 DAR ES SALAAM.

CAB 157/547/01/C/47

Kumb. Na.....

02 Januari, 2015

WARAKA WA MKUU WA UTUMISHI WA UMMA
NA. 1 WA MWAKA 2015

KUHUSU UTARATIBU KWA WATUMISHI WA UMMA
WANAOGOMBEA NYADHIFA ZA KISIASA NCHINI

1.0 UTANGULIZI:

- 1.1 Mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yaliyofanyika Julai, 1992 yaliruhusu mfumo wa vyama vingi vya siasa kutumika nchini. Kufuatia mabadiliko hayo, Serikali ilitoa mwongozo wa kuelekeza namna watumishi wa umma watakvoyoshiriki katika shughuli za kisiasa, kupitia Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na. 1 wa Mwaka 1992.
- 1.2 Uzoefu wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1995 na chaguzi za Serikali za Mitaa za mwaka 1994 na 1999 ulionesha kuwa ushiriki wa watumishi wa umma katika shughuli za siasa uliathiri maadili ya msingi ya utendaji kazi Serikalini na kwenye vyombo vyake. Hivyo, kutokana na kasoro hizo, Serikali ilihusha Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na.1 wa mwaka 1992 na kutoa Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na.1 wa mwaka 2000.
- 1.3 Pamoja na kuhuisha Waraka huo, bado kulikuwa na baadhi ya changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji, na hivyo kusababisha kutolewa kwa marekebisho Namba 1, 2 na 3 kwa Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na.1 wa mwaka 2000.
- 1.4 Pamoja na utekelezaji wa Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na. 1 wa mwaka 2000, na marekebisho yake, kumekuwepo bado na malalamiko na changamoto mbalimbali, ikiwa ni pamoja na:
 - 1.4.1 Watumishi wa umma ambao pia wana nafasi za kisiasa wameendelea kutumia muda mwingi wa waajiri wao kufanya shughuli za kisiasa katika maeneo yao ya uongozi na hivyo kuathiri majukumu yao ya kiutendaji;

